2. **TAMTHILIA**

KITHAKA WA MBERIA: Kifo Kisimani

Jibu swali 2 au la 3

"Kwa bahati nzuri utawala ulituhakikishia kwamba hatungepata shida yoyote…."

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

b) Fafanua 'shida' aliyohakikishiwa hawangepata. (alama 4)

c) Fafanua njia sita ambazo utawala ulitumia kuendeleza shida zilizowakumba wana Butangi. (alama 12)

3. Huku ukirejelea tamthilia ya Kifo Kisimani, eleza jukumu la vijana katika jamii. (alama 20)

HADITHI FUPI

K.W. WAMITILA; Mayai waziri wa maradhi

Jibu swali la 4 au la 5

4. "Au ataka mahari yarudishwe? Kiingiacho kwa mganga hakitoki babu".

a) Eleza muktadha wa kauli hii. (alama 2)

b) Taja mbinu mbili zilizotumika katika dondoo hili na ueleze. (alama 2)

c) Onyesha jinsi mwanamke alivyodhahilishwa katika hadithi husika. (alama 10)

d) Rejelea na ufafanue athari sita za kudhalilishwa huku. (alama 6)

5. Janga lililokumba shule ya Angeko lilitokana na kutowajibika. Huku ukirejelea hadithi ya ndimi za mauti thibitisha ukweli huu. (alama 20)

6. **USHAIRI**

Soma shairi hili kisha ujibu maswali

Sema semea wajibu, ewe mwenye kutetema
Sema na walo karibu, na wa mbali ukisema
Sema kufunza wajibu, werevu au hekima
Sema asikie nani, mlimwengu asokoma.

Sema yanayokukaa, yaliyo kukusakama
Sema yaliyozagaa, uwambie kuungama
Sema unajihadaa, wadhani yatawafuma
Sema asikie nani, usiyejua kusema

Sema semea uasi, na hizi nyingi zahama
Sema toa wasiwasi, utarajie salama
Sema neno la risasi, lipenyalo likiuma
Sema asikie nani, usiyejua kusema

Sema bila ya ukali, bembeleza ukisema
Sema neno la asali, wataramba wakitema
Sema tumia akili, kwao hukosi shutuma
Sema iwe jambo gani, mlimwengu asokoma

Sema zitaje ghururi, dunia ni kama dema
Sema haiweki siri, inavuja ikitema.
Sema dunia hatari, mtendayo yatuuma
Sema ajaliye nani, mlimwengu hana wema.

Sema na katu sisemi, kwa asojua kupima
Sema awe ni mtemi, asojua nilosema
Sema miko yangu mimi, sisemi neno daima
Sema niseme na nani, ili iweko salama

a) Taja na ueleze aina nyinginezo tatu za habari za shairi hili bali na tarbia. (alama 6)
b) Toa mifano miwili ya maneno yaliyoandikwa kishairi na kisha uyaandike kisanifu. (alama 2)
c) Toa mifano mwafaka kushuhudia kuwa shairi lina ujumbe wa kukatisha tamaa. (alama 4)
d) Andika ubeti wa nne katika lugha ya nathari. (alama 4)
e) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi. (alama 4)
(i) Yaliyozagaa
(ii) Dema
(iii) Ghururi
(iv) Zahama

FASIHI SIMULIZI

(a) Eleza maana ya tanzu zifuatazo. (alama 6)
(i) Vitendawili
(ii) Ngano
(iii) Vitanza ndimi

b) Eleza sifa za
- Vitendawili. (alama 4)
- Ngano (alama 6)
- Vitanza ndimi. (alama 4)

Mwisho